**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

# TAARIFA KUHUSU PATO LA TAIFA KWA ROBO MWAKA YA KWANZA JANUARI – MACHI, 2014

**Ofisi ya Taifa ya Takwimu**
**Wizara ya Fedha**
**Septemba, 2014**

## 1.0 Utangulizi


Taarifa za takwimu za Pato la Taifa kwa robo mwaka zinatumika katika kutathmini mabadiliko ya ukuaji wa uchumi katika vipindi vifupi vya robo mwaka. Taarifa hii ni kwa kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Machi, 2014.

Taarifa zilizotumika kutayarisha takwimu za Pato la Taifa zimetokana na uzalishaji wa bidhaa na huduma Nchini katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2014. Aidha, ukokotoaji wa takwimu za Pato la Taifa umezingatia matakwa ya Mfumo wa Umoja wa Mataifa wa ukokotoaji wa takwimu za Pato la Taifa (UN System of National Accounts).

## 1.1 Ukuaji wa Pato la Taifa

Ukuaji wa Pato la Taifa kwa bei ya soko uliongezeka kwa kasi ya asilimia 7.4 katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2014 ikilinganishwa na kasi ya asilimia 7.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2013, Kielelezo Namba 1. Jumla ya thamani ya Pato la Taifa katika kipindi husika ilikuwa Shilingi 4,862,689 milioni mwaka 2014 ikilinganishwa na Shilingi 4,526,148 milioni mwaka 2013.

**Kielelezo Namba 1: Kasi ya Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Robo Mwaka, Robo ya Kwanza, Januari – Machi, 2004 – 2014**



## 2.0 Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Shughuli Mbalimbali za Kiuchumi

Mchanganuo wa ukuaji wa shughuli za kiuchumi kwenye Pato la Taifa kwa robo mwaka ya kwanza 2014 ni kama ifuatavyo:

### 2.1 Kilimo na Uvuvi

Shughuli za kiuchumi za kilimo zilifikia kasi ya ukuaji ya asilimia 1.6 katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2014 ikiwa ni kasi sawa na iliyofikiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2013.

Katika kipindi hicho, Shughuli za Kilimo cha Mazao zilikua kwa asilimia 1.4 mwaka 2014 ikilinganishwa na asilimia 0.6 mwaka 2013; Shughuli za Mifugo zilikua kwa asilimia 1.8 mwaka 2014 ikilinganishwa na asilimia 3.5 na Shughuli za Misitu na Uwindaji zilikua kwa asilimia 1.6 mwaka 2014 ikilinganishwa na asilimia 2.9 mwaka 2013. Aidha, katika kipindi hicho kulikuwa na mvua za kutosha katika maeneo yanayozalisha mazao kwa wingi. Aidha, maelekezo ya ma-ofisa Ugani kwa wakulima kama kuchagua aina bora ya mbegu yalisaidia kuongeza uzalishaji.

Shughuli za uvuvi zilikua kwa kasi ya asilimia 2.5 katika robo ya kwanza ya mwaka 2014 ikilinganishwa na asilimia 1.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2013. Kasi ya ukuaji huu ilitokana na kuongezeka kwa uvunaji wa samaki ili kukidhi mahitaji ya samaki katika soko la ndani na soko la kimataifa.

### 2.2 Viwanda na Ujenzi

Shughuli za uchimbaji madini, mawe na kokoto ziliongezeka na kufikia kasi ya asilimia 8.7 katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2014 ikilinganishwa na kasi ya ukuaji wa asilimia hasi 1.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2013. Kuongezeka kwa kasi hii ya ukuaji ilitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa madini ya dhahabu katika robo ya kwanza ya mwaka 2014.

Shughuli za uzalishaji bidhaa viwandani zilifikia kasi ya ukuaji ya asilimia 8.5 katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2014 ikilinganishwa na kasi ya asilimia 8.3 mwaka 2013. Kuongezeka kwa kasi ya ukuaji ya asilimia 0.2

kulitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa za vyakula, vinywaji na bidhaa za tumbaku.

Shughuli za uzalishaji nishati ya umeme na usambazaji maji zilikua kwa kasi ya asilimia 12.6 katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2014 ikilinganishwa na kasi ya asilimia 6.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2013. Kuongezeka kwa ukuaji wa nishati ya umeme na maji kulitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa nishati ya umeme unaotokana na mafuta na gesi.

## 2.3 Shughuli za Uchumi za Utoaji Huduma

Shughuli za biashara za jumla na reja reja, ukarabati wa magari na pikipiki na vifaa vingine vya majumbani zilifikia kasi ya ukuaji wa asilimia 8.0 katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2014 ikilinganishwa na kasi ya asilimia 10.0 katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2013. Shughuli za upangishaji nyumba, na shughuli zingine za biashara zilifikia kasi ya ukuaji wa asilimia 8.1 ukilinganisha na asilimia 9.0 katika kipindi kama hicho mwaka 2013.

Shughuli za uchukuzi na mawasiliano zilifikia kasi ya ukuaji wa asilimia 16.5 katika kipindi husika. Shughuli nyingine ni huduma za Hoteli na migahawa zilizofikia kasi ya ukuaji wa asilimia 3.0; Shughuli za uendeshaji Serikali zilifikia kasi ya asilimia 5.1, Elimu asilimia 5.2 na huduma za Afya na shughuli nyinginezo zilifikia kasi ya ukuaji wa asilimia 4.5 katika kipindi hicho.

## 3.0 Hitimisho

Pato la Taifa limetayarishwa kutokana na taarifa zilizokusanywa kutoka katika shughuli za kiuchumi katika kipindi cha Januari hadi Machi 2014, na limekua kwa asilimia 7.4 ikilinganishwa na asilimia 7.1 katika kipindi cha Januari hadi Machi, 2013.

Kwa mujibu wa maoteo kutoka ”Financial Programming Group”, ukuaji wa uchumi unatarajiwa kufikia asilima 7.2 katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2014.

Aidha, Ofisi ya Taifa ya Takwimu itasambaza takwimu za Pato la Taifa kwa robo mwaka ya pili (Aprili – Juni, 2014) tarehe 30 Septemba, 2014 kama ilivyo kwenye shajala ya machapisho ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu.